

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA MISSENYI



UMOJA NI USHINDI



Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi
S.L.P 38, KYAKA
(+255) 784 84 96 99/ (+255) 756 58 30 37
Barua Pepe: ded@missenyidc.go.tz
Tovuti: www.missenyidc.go.tz



**TAARIFA YA MAFANIKIO YA UTEKEREZAJI WA ILANI
YA CHAMA CHA MAPINDUZI KWA KIPINDI CHA
MIAKA MITANO 2015-2020**



*"Tunaendelea kufungua njia ya Maendeleo
Endelevu ya Wanamissenyi".*

JUNI, 2020



Mhe. Frank Theophil Muganyizi
Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Missenyi.



Mhe. Knl. Denis Filangali
Mwila
Mkuu wa Wilaya ya Missenyi.



Mhe. Balozi Dkt. Diodorus
Buberwa Kamala
Mbunge wa Jimbo la Nkenge



Ndugu
Abdallah Ramadhani
Mayomba
Katibu Tawala Wilaya ya
Missenyi.



Mhe. Projectus Kweyamba
Tegamaisho
Mwenyekiti wa Halmashauri
ya Wilaya ya Missenyi.



Ndugu Innocent Mbandwa Mukandala
Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya
Missenyi.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



HALMASHAURI YA WILAYA MISSENYI



**TAARIFA YA MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA ILANI
YA CHAMA CHA MAPINDUZI KWA KIPINDI CHA MIAKA
MITANO 2015 - 2020**



JUNI, 2020

YALIYOMO


YALIYOMO	ii
ORODHA YA MAJEDWALI.....	iii
1.0 Dibaji	iv
1.0 UTANGULIZI	1
2.0 UKUAJI WA UCHUMI.....	4
2.1 Bajeti ya Halmashauri	4
2.2 Mapato ya ndani	4
3.0 SEKTA ZA UZALISHAJI MALI.....	6
3.1 Kilimo na Ushirika	6
3.1.1 Kilimo	6
3.1.2 Ushirika.....	8
3.2 Mifugo na Uvuvi	8
3.2.1 Mifugo	9
3.2.2 Uvuvi.....	10
3.3 Maliasili.....	11
3.4. Usafi na Mazingira	12
3.4 Viwanda na Biashara	13
4.0 HUDUMA ZA KIUCHUMI.....	15
4.1 Ardhi	15
4.1.1 Utawala wa Ardhi:	15
4.2 Barabara	15
4.3 Nishati ya Umeme	16
5.0 HUDUMA ZA JAMII.....	17
5.1 Afya	17
5.2 Elimu.....	19
5.2.1 Elimu Msingi.....	19
5.2.1.1 Elimu ya Awali.....	19
5.2.1.2 Elimu ya Msingi	19
5.2.1.3 Elimu ya Mafunzo ya Ufundı	21
5.2.2 Elimu ya Sekondari	21
5.3 Maji	23
6.0 UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI	25
6.1 Kuwezesha sekta binafsi.....	25
6.2 Kuwatambua Wajasiliamali na kuwawezesha mikopo	25
6.3 Kuwawezesha Vijana Kujajiri.....	26
6.4 Kuwezesha Kaya Maskini	27
7.0 MAFANIKIO YA UTAWALA BORA NA DEMOKRASIA.....	29
7.1 Utumishi na Utawala	29
7.2 Ushiriki wa Vyama vya siasa katika Wilaya	29
7.3 Uchaguzi wa Serikali za Mitaa	29
7.4 Maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020	30
8.0 CHANGAMOTO	30
9.0 HITIMISHO	30

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 1: Mapato ya Halmashauri kwa miaka Mitano.....	5
Jedwali 2: Uzalishaji wa mazao ya Miwa na Kahawa	6
Jedwali 3: Upandaji miti kuanzia 2015 - 2020	11
Jedwali 4: Maeneo yaliyotengwa kwa uwekezaji.....	13
Jedwali 5: Vikundi viliyyopatiwa mikopo kuanzia 2015-Machi 2020.....	26
Jedwali 6: Miradi ya maendeleo kwa kila Kata	31- 62
Jedwali 7: Mikopo kwa Vikundi vya Vijana, Wanawake na Walemavu	63 - 74



HALMASHAURI YA WILAYA MISSENYI KWA UFUPI



Halmashauri ya Wilaya Misserenyi ilianzishwa mwaka 2007 baada ya kugawa Halmashauri ya Wilaya Bukoba, na ni mionganoni mwa Halmashauri **nane** za Mkoa wa Kagera. Halmashauri zingine ni: Biharamulo, Bukoba, Bukoba Manispaa, Karagwe, Kyerwa, Muleba na Ngara. Wilaya Misserenyi iko upande wa Kaskazini Magharibi mwa Mji wa Bukoba na imepakana na Ziwa Victoria kwa upande wa Mashariki, Halmashauri ya Bukoba kwa upande wa Kusini, Halmashauri ya Kyerwa kwa upande wa Magharibi na Nchi ya Uganda kwa upande wa Kaskazini.

Wilaya ya Misserenyi ina jumla ya eneo lipatalo hekta **270,876**, na kati ya hekta hizo, jumla ya hekta **99,726** zinatafaa kwa kilimo na hekta **63,884** ni kwa ajili ya malisho ya mifugo. Kwa sasa eneo linalotumika kwa kilimo ni hekta **59,840** na hekta **31,547** ni maeneo ya misitu ya hifadhi, sehemu kubwa ikiwa ni Hifadhi ya Misitu ya: Minziro, Mnene, Kikuru, Lwasina, Kantare, Kikongoro, Ruchwezi na Bushenya.

Kwa mujibu wa Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, Wilaya ya Misserenyi ina watu **202,632** (Wanawake ni **102,547** na Wanaume ni **100,085**) na Kaya **35,699**. Wilaya ya Misserenyi ina Kanda mbili za mvua: Tarafa ya Misserenyi inayopata mvua nydingi (**mm 1,400 – 2,000**) na Tarafa ya Kiziba inayopata mvua ya wastani (mm 600 – 1,000). Wilaya ina wastani wa nyuzi joto kati ya **15°C** na **28°C**.

Wilaya ya Misserenyi imegawanyika katika Tarafa **mbili** za: Misserenyi na Kiziba, Kata **20**, Vijiji vilivyosajiliwa **77** na Vitongoji **356**.

Takribani asilimia **90** ya Wakazi wa Halmashauri ya Misserenyi hujishughulisha na Kilimo na Ufugaji, asilimia **tano** ni Wavuvi na asilimia **tano** ni Waajiriwa na Wafanya biashara. Ufugaji wa nyuki kando kando ya Misitu na biashara ya mbao ni mionganoni mwa shughuli za kiuchumi zinazokua kwa kasi kwenye Halmashauri ya Wilaya Misserenyi Aidha, kilimo cha umwagiliaji, kilimo cha miwa, mpunga na alizeti ni mionganoni mwa shughuli za kiuchumi ziazoendelea kuhimizwa na kupata mwitikio chanya.

Wakazi wengi walioajiriwa wanafanyakazi kwenye kiwanda cha sukari (Kagera Sugar Co.), Taasisi za Serikali na Watu binafsi zilizomo kwenye Halmashauri. Wafanya biashara wengi wako kwenye Miji ya Bunazi, Kyaka na Mutukula ambayo inakuwa kwa kasi kubwa. Pamoja na shughuli zinazoendelea, kuna fursa nydingi za Uwekezaji, hasa kwenye nyanja za Viwanda, Kilimo, Ufugaji, Biashara mipakani na Utalii katika hifadhi na makumbusho ni kumbukumbu ya vita ya Kagera.



1.0 UTANGULIZI

Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015, ni mkataba baina ya CCM na Wananchi wa Tanzania waliokubali kukichagua chama cha mapinduzi (CCM) kutokana na imani kubwa waliyokuwa nayo juu ya uwezo wa utekelezaji wa ahadi zake zilizoainishwa katika Ilani hiyo dhidi ya Ilani nyingine za vyama vyamia upinzani zilizonadiwa kwa wananchi.

Ilani hii ilinadiwa na aliyekuwa Mgombea Mahiri wa CCM dhidi ya ilani za wagombea wa vyama vyamia upinzani. Serikali ya Awamu ya Tano kuitia Chama cha Mapinduzi iliingia madarakani Novemba, 2015, chini ya Uongozi wa Mhe. Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kipindi chote cha miaka mitano, Serikili imefanya kazi kubwa katika kuhakikisha huduma za Kiuchumi na Kijamii zinaimarika, zinatekelezwa na kutolewa katika mamlaka za Serikali za Mitaa.

Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi ikiwa miongoni mwa Halmashauri **185** za Tanzania bara yenye idadi watu 202,632 kulingana na sensa ya mwaka 2012, Halmashauri hii imefanya kazi kubwa ya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015 -2020 katika maeneo ya sekta mbalimbali za Kiuchumi na Kijamii.

Halmashauri imeafanikiwa kuongeza makusanyo ya Mapato yake ya ndani kutoka **Tsh. 1,135,686,580.00** za Mwaka 2015/2016 hadi kufika Tsh. **2,448,152,629.72** Mei, 2020 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia **116**. Mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri imepitisha bajeti ya Tshs. **3,041,629,000.00** ikiwa ni ongezeko la asilimia **23** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2019/2020. Ongezeko hili la Mapato limeiwezesha Halmashauri kupungaza utegemezi wa fedha kutoka Serikali kuu kutoka asilimia **90** ya mwaka 2015/2016 hadi kufikia asilimia **79** kwa mwaka 2019/2020.

Kilimo ni sehemu kubwa ya shughuli za kiuchumi katika Wilaya ambacho kimeimarika kwa kuongezeka kwa uzalishaji wa Mazao ya biashara na Chakula kutoka tani **222,914.5** hadi kufikia tani **282,544.3** sawa na asilimia **27**. Aidha, Mazao **tatu** mapya ya Vanila, Mpunga na Alizeti yameanzishwa na kuawezesha wakulima kutanua wigo wa Kilimo katika Wilaya ya Missenyi.

Uboreshaji wa huduma za ugani kwa wafugaji umefanyika na kufanikisha kuongeza idadi ya mifugo kutoka **93,067** Mwaka 2015 hadi kufikia **105,159** mwaka 2020 sawa na asilimia **13**. Hivyo, ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali umeongezeka. Hali ya utunzaji na uhifadhi wa Mazingira katika Wilaya umeongezeka kutoka asilimia **54** mwaka 2015 hadi kufikia asilimia **85** mwaka 2020. Miti **11,084,302** imepandwa na Mizinga ya kisasa **1,264** imetengenezwa na kugawanya kwa vikundi na watu binafsi. Aidha, migogoro ya wafugaji katika huria ya Missenyi imetatuliwa yote.

Hatua za kuandaan mipango ya matumizi bora ya Ardhii kwa lengo la kuondoa migogoro zimeendelea kuchukuliwa kwa kupima na kutoa hati miliki kwa wakulima na wawekezaji. Jitihada hizo zimewesha upimaji wa jumla ya ekari **14,300** za mashamba. Katika kuhakikisha utekelezaji wa sera ya Uchumi wa Viwanda eneo la Hekta **5,250.5** imetengwa kwa ajili ya shughuli za Viwanda, Biashara na Kilimo ili kuvutia uwekezaji huo.



Wilaya imefanikiwa kuwa na mtando wa barabara zenyе urefu wa Km **921.16** kati ya hizo baraba za kiwango cha lami ni Km. **1.5**, Changarawe ni Km **260** na Udongo ni Km **659.66**. Barabara zenyе urefu wa jumla ya kilometra **656.93** zimekuwa katika hatua mbalimbali za ujenzi ambapo jumla ya barabara zenyе urefu wa kilometra **621.93** zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha udongo na changarawe.

Kiwango cha uunganishwaji umeme Vijijini kiwilaya umeongezeka kutoka Vijiji **26** sawa na asilimia **33.7** mwaka 2015 hadi kufikia Vijiji **72** sawa na asilimia **93.5** mwaka 2020. Jumla ya nyumba za makazi **3,326** nyumba za ibada **26** Shule **43** na Zahanati **11** zimeunganishiwa huduma ya umeme kwa gharama nafuu.

Huduma za Afya zimeendelea kuimarishwa hususani kupunguza vifo vy'a mama wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano, kutokana na kuongezwa kwa bajeti ya Madawa na Vifaa tiba kutoka Tsh. **281,763,765.00** na hadi kufikia Tsh. **593,837,525.60**. Vile vile, Ujenzi na Ukarabati wa Kituo cha Afya Bunazi umetumia Tsh, **437,950,350.00** na Ujenzi wa kituo kipy'a cha Afya Kabyaile.

Ruzuku ya Wanafunzi (Capitation Grants) kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vy'a kufundishia na kujifunzia; Fidia ya ada; Posho za Madaraka kwa Walimu Wakuu **96**, Wakuu wa Shule **22** na Maafisa Elimu **20** imeendelea kutolewa. Ruzuku hiyo ya Tsh. **3,271,171,993.72** ya Elimu bila malipo imetolewa tangu kuanzishwa Desemba, 2015 hadi Aprili, 2020. Kati ya hizo Tshs **1,922,702,700.72** ni za Elimu Msingi na **Tsh.1,348.469,293** ni za Elimu Sekondari.

Jitihada hizi zimeenda sambamba na Idadi ya vyumba vy'a maabara kuongezeka kutoka **saba** mwaka 2015 hadi **46** mwaka 2020 na maabara **20** zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Aidha mahitaji ya vyumba vy'a maabara kwa shule **22** za Sekondari ni **66**.

Wilaya imeendelea kuimarisha huduma za maji Vijijini kwa kukarabati, kujenga na kupanua miundombinu ya maji, hali iliyochangia upatikanaji wa huduma ya Maji Safi na Salama Vijijini na kuongezeka kutoka asilimia **58** mwaka 2015 hadi kufikia asilimia **71** mwaka 2020.

Muunganisho wa Ujasiriamali Vijijini kwa Wanawake, Vijana na Walemau Umewezeshwa na kufanikiwa, ambapo mikopo yenye jumla ya Tshs. **501,995,546.00** imetolewa na kuwanufaisha wananchi **3,302** katika vikundi **262** kutoka sehemu mbalimbali ndani ya Wilaya. Vile vile Serikali kupitia mradi wa TASAF, imelipa ruzuku Tshs. **5,141,704,500** kwa Kaya maskini **6,292** wilayani ambapo hali ya maisha ya walengwa hawa imepanda.

Katika kuhakisha huduma kwa wananchi inatolewa kwa ufanisi, Watumishi wa kada mbali mbali wameongezeka kutoka **1,326** Mwaka 2015/2016 hadi kufikia Watumishi **1,687** kwa mwaka 2019/2020 na kufanya Watendaji wa kata zote **20** kuwa na sifa za kumuundo. Ongezeko hili ni sawa na asilimia **27**.



Kwa kipindi hiki cha miaka **mitano** Halmashauri imeweza kutekeleza miradi ya maendeleo **430** yenye thamani ya Tsh.**14,366,582,275.74**, ikiwa miradi ya serikali kuu Tshs. **7,078,818,000**, Miradi ya mapato ya ndani Tshs. **2,812,425,954.00**, Miradi ya wadau wa maendeleo Tshs. **2,280,719,715.00**, miradi ya Mfuko wa Jimbo Tshs. **255,340,000.00** na Tshs. **1,939,278,606.74** ikiwa ni michango ya jamii kwenye miradi ya maendeleo.

Halmashauri imepata hati safi kwa miaka **minne** mfululizo 2015/2016 hadi 2018/2019. Aidha, Vikao **123** vya Baraza la Madiwani vimefanyika sawa na asilimia **100**, Vikao **400** vya Maendeleo ya Kata (WDC) vimefanyika sawa na asilimia **100** na Mikutano mikuu **1,324** ya Vijiji imefanyika sawa na asilimia **86**.

Mafanikio yaliyopatikana yametokana na juhudini kubwa zilizofanywa na viongozi katika ngazi zote kwa kushirikiana, Vyama vya siasa, Wananchi na wadau wa maendeleo. Huu ndio msingi wa Dhana ya Utawala Bora ya kuendelea kutekeleza Mikakati na Mipango shirikishi ilioanzishwa kwa maslahi mapana ya wananchi wote na Taifa kwa ujumla. Watanzania wote wana wajibu wa kuyaenzi mafanikio haya yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitano na kufanya kazi kwa bidii ili kujilettea mafanikio zaidi.

Taarifa hii ina sura **sita** ambazo zimeelezea kwa kina mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa kipindi cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano katika maeneo ya Ukuaji wa Uchumi, Sekta za Uzalishaji Mali, Huduma za Kiuchumi, Uwezeshaji Wananchi na Huduma za Jamii.

Hapa kazi tu.



2.0 UKUAJI WA UCHUMI

2.1 Bajeti ya Halmashauri

Makisio ya bajeti ya Halmashauri imeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka kutoka Tshs **21,565,000,353.95** mwaka 2015/2016 na kufikia Tshs **25,257,247,645.00** mwaka 2019/2020 ambalo ni ongezeko la Tshs. **3,692,247,291.05** sawa na asilimia **17**. Mafanikio ya ongezeko hili limetokana na usimamizi na ufuatiliaji imara wa Uongozi wa Wilaya kwa kuweka mikakati madhubuti ya kuongeza vyanzo vya mapato ya ndani na kusimamia fedha za Serikali Kuu pamoja na za Wadau wa Maendeleo kwa ufanisi na tija wakizingatia Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya fedha za Umma.

2.2 Mapato ya ndani

Mapato ya ndani ni Sehemu kuu ya bajeti ya Mapato na matumzi ya Halmashauri. Makisio ya bajeti ya Mapato ya ndani yameongezeka kutoka Tsh. **1,233,744,000.00** mwaka 2015/16 hadi kufikia Tsh. **2,467,613,000.00** kwa Mwaka 2019/2020, ongezeko hili ni sawa na asilimia **100**. Ukusanyaji wa Mapato ya ndani ya Halmashauri kwa kuzingatia makisio haya ya makusanyo yameongezeka kutoka Tshs. **1,135,686,580.00** mwaka 2015/2016 hadi kufikia Mei, 2020 ni Tshs. **2,448,152,629.72** sawa na asilimia **116** kwa mwaka 2019/2020.

Malengo ya makusanyo ya bajeti ya mapato ya ndani yamekuwa yakifikiwa kwa zaidi ya wastani wa asilimia **80** kwa kila mwaka. Halmashauri mwaka wa fedha 2020/2021 imepitisha makisio ya bajeti ya Tshs. **3,041,629,000.00** sawa na ongezeko la Tsh. **1,807,885,000**. Ongezeko hili ni sawa na asilimia **147** ya maksio ya bajeti ya mwaka 2015/2016.

Mafanikio haya yamechangiwa na hatua madhubuti zinazoendelea kuchukuliwa na Halmashauri katika kuimarisha mfumo wa usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya ndani yasiyofungiwa na fungiwa, kuziba mianya ya upotevu wa mapato ya ndani kwa kutumia mfumo wa kielectroniki wa ukusanyaji wa Mapato ya ndani, kutambua vyanzo vipyta, kuhuisha vyanzo vya zamani, kuondoa mawakala wa ukusanyaji, kutumia watumishi wa Serikali na Vibarua waadilifu katika ukusanyaji wa Mapato, uandaaji wa kanzi data ya vyanzo vya mapato ya Halmashauri, kuimarisha kikosi kazi cha ukusanyaji mapato, ukaguzi wa mara kwa mara kwa wafanyabiashara na vizuizi vya kukusanya mapato barabarani/kwenye njia kuu na vile vile kuimarika kwa shughuli za kiuchumi katika Wilaya.

Ongezeka la mapato ya ndani ya Halmashauri kwa kila mwaka kumeweza kupunguza utegemezi wa bajeti ya mapato na Matumizi kwa kutoka asilimia **90** kwa mwaka 2015/2016 hadi kufikia asilima **79** ya mwaka 2019/2020, vile vile kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo kuitia asilimia **40** ya makusanyo yote yaliyopatikana kwa kipindi husika na kuimarisha uendeshaji wa shughuli za Ofisi. Aidha, Kiasi cha Tshs. **2,812,425,954** za mapato ya ndani kimepelekwa kwenye miradi ya maendeleo kwa kipindi cha Mwaka 2015/2016 hadi 2019/2020.



**TAARIFA YA MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI
KWA KIPINDI CHA MIAKA MITANO 2015-2020**

Jedwali 1: Mchanganuo wa Mapato ya Ndani Halmashauri kwa Miaka Mitano.

Mwaka wa Fedha	Makisio	Mapato ya Halmashauri 2015/2020	Asilimia
2015/2016	1,233,744,000.00	1,135,686,580.00	92
2016/2017	1,630,203,000.00	1,597,121,992.00	98
2017/2018	1,902,733,210.00	1,473,938,786.00	77
2018/2019	2,467, 613,000.00	2,136,689,004.17	87
2019/2020	2,467, 613,000.00	2,480,130,014.72 hadi 28/05/2020.	100



3.0 SEKTA ZA UZALISHAJI MALI

3.1 Kilimo na Ushirika

Idara ya Kilimo na Ushirika imeendelea kutoa huduma za ugani, utunzaji wa mazingira, udhibiti wa maafa na kuimarisha usimamizi wa shughuli za Ushirika. Huduma hizi zimewezesha kuwajengea uwezo wakulima kwa kuendesha Kilimo biashara chenye uzalishaji wenye tija kila mwaka na kuongezeka kwa shughuli za ushirika katika Wilaya.

3.1.1 Kilimo

Katika kipindi cha miaka mitano, Halmashauri iliweka Kipaumbele cha kuhakikisha kuwa kilimo katika Wilaya kinakuwa endelevu na chenye tija ili kuwawezesha wananchi kujitosheleza kwa chakula, kuongeza kwa mapato ya wakulima, kuwa chanzo cha kuaminika cha malighafi ya sekta ya viwanda na kuendelea kuwa chanzo kikuu cha ajira kwa wananchi. Kwa kutekeleza azma hiyo, mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

- i. Katika kuimarisha huduma za ugani, idadi ya maafisa ugani katika ngazi ya Kata na Vijiji imeongezeka kutoka **25** mwaka 2015/16 hadi **30** mwaka 2019/2020 sawa na asilimia **20**.
- ii. Uzalishaji wa zao la miwa umeongezeka kutoka Tani **70,028.5** mwaka 2015/2016 hadi kufikia Tani **80,000** mwaka 2019/2020
- iii. Uzalishaji wa zao la Kahawa umeongezeka kutoka Tani **428.9** kwa mwaka 2015/2016 hadi kufikia Tani **910.8** kwa mwaka 2019/2020 kama jedwali Na. **2** linavyoonesha.

Jedwali Na. 2: Uzalishaji wa Mazao ya Miwa na Kahawa

Namba	Mwaka	Miwa (Tani)	Kahawa (Tani)
1	2015/2016	51,063.3	428.9
2	2016/2017	56,201.8	181
3	2017/2018	59,643.6	626.4
4	2018/2019	42,834.4	1,604
5	2019/2020	80,000 (makisio)	910.8



- iv. Matumizi ya mbolea za viwandani yameongezeka kutoka Tani **91.2** mwaka 2015/16 hadi Tani **114** mwaka 2019/20 sawa na ongezeko la asilimia **25**.
- v. Kiwango cha uzalishaji wa mazao ya chakula kimeendelea kuongezeka kutoka Tani **152,886** mwaka 2015/2016 hadi Tani **202,544.3** mwaka 2019/20 ambapo ni sawa na ongezeko la asilimia **14**. Ongezeko hili limeiwezesha Wilaya kujitosheleza kwa chakula na ziada kuuzwa nje ya Wilaya.
- vi. Katika juhudi za kuhifadhi mazao kwa ubora unaostahili, jumla ya maghala mawili yaliyopo kata za **Kilimilile** na **Mushasha** yenyewe uwezo wa kuhifadhi kati ya Tani **40** hadi **45** yamekarabatiwa. Aidha, ujenzi wa ghala lenye uwezo wa kuhifadhi Tani **20** umekamilika katika kata ya Kassambya. Kwa sasa Wilaya ina maghala **manne**.
- vii. Hatua za kuongeza thamani ya mazao ya kilimo cha mboga mboga na matunda zimechukuliwa kwa kujenga kitalu Nyumba “Green house” yenyewe thamani ya milioni ishirini na sita (**Tshs 26,000,000**) ndani ya eneo la ofisi za Halmashauri.
- viii. Hatua ya kuongeza mnyororo wa thamani ya mazao imetekelizwa kwa kutoa mashine **mbili** za kusindika na kusafisha mafuta ya alizeti kwa vikundi **viwili** vya wazalishaji na wasindikaji wadogo ambavyo ni **Shubira** na **Rashana** katika kata za Kilimilile na Kitobo ili kuongeza thamani ya zao la Alizeti.
- ix. Wakulima wa Miwa wa nje ya kiwanda (outgrowers) wameongezeka kutoka **362** mwaka 2015/2016 hadi kufikia Wakulima **525** mwaka 2019/20, kutokana na ongezeko hilo la wakulima, uzalishaji wa miwa umeongezeka kutoka Tani **70,028.5** zenye thamani ya Tshs **3,270,332,818.00** kwa mwaka 2015/2016 na kufikia maksio ya tani **80,000** zenye thamani ya Tshs **4,800,000,000.00** kwa mwaka 2019/2020.
- x. Wakulima wa Miwa wa nje ya kiwanda (outgrowers) wameeweza kulipa ushuru (crop cess) kutoka Tshs **32,703,328.18** mwaka 2015/2016 hadi Tshs. **144,000,000.00** kwa mwaka 2019/2020, Ongezeko hili la ushuru ni sawa na ongezeko la asilimia **63**.



Shamba la Miwa katika kata ya Kassambya

- xii. Wakulima wameweza kujifunza na kutangaza mbinu bora za kilimo kupitia kupelekwa kwa wawakilishi wa wakulima hao katika sherehe za wakulima Kimkoa na kikanda kwa kipindi chote cha miaka mitano. Wakulima wameweza kuiletea Halmashauri ushindi wa Kimkoa kwa miaka minne kati ya mitano sawa na asilimia **80** na mara moja kupata mkulima mmoja bora kikanda.
- xiii. Kumekuwepo Uanzishwaji na uzalishaji wa Mazao mapya ndani ya wilaya.
- a. **Vanila:** Uzalishaji wa zao la Vanila umeongezeka kutoka Miche **40,401** mwaka 2015 hadi Miche **101,111** mwaka 2020 sawa na asilimia **150**.
 - b. **Mpunga:** Uzalishaji wa zao la Mpunga umeongezeka kutoka Hekta **12** mwaka 2015 hadi **39.04** mwaka 2020 sawa na asilimia **225**.
 - c. **Alizeti:** Uzalishaji wa zao la Alizeti umeongezeka kutoka hekta **12** mwaka 2015 hadi hekta **31** mwaka 2020 sawa na asilimia **158**.



Shamba la mpunga Katebe Mutukula



Shamba la vanilla Mugongo Kata ya Ruzinga

3.1.2 Ushirika

Kitengo cha Ushirika kilicho chini ya Tume ya Maendeleo ya ushirika kimeendelea kuimarisha usimamizi wa Sekta ya Ushirika katika Wilaya ambapo mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

- i. Idadi ya vyama vya ushirika imeongezeka kutoka vyama **73** mwaka 2015/2016 vyenye wanachama **5,558** hadi vyama **78** kwa mwaka 2019/2020, vyenye wanachama **8,176**.
- ii. Makusanyo ya mazao ya kimkakati hususani kahawa kupitia vyama vya Ushirika yameongezeka kutoka wastani wa Tani **428.9** (2015/2016) hadi wastani wa Tani **1,604** (2018/2019) sawa na ongezeko la Tani **1,175.1** ambayo ni asilimia **274**



Wajumbe wa bodi wa Chama cha ushirika MVIWAKE AMCOs toka kenyana wakipata mafunzo ya uongozi na sheria.

3.2 Mifugo na Uvuvi

Katika kipindi cha miaka mitano, Sekta ya Mifugo na Uvuvi imeimarika na hivyo kuongeza uzalishaji wa mazao ya mifugo na samaki ambayo yameongeza makusanyo ya Serikali kuu, mapato ya ndani ya Halmashauri, Wafugaji na Wavuvi pamoja na kuchangia ukuaji wa Pato la Mwananchi wa Wilaya ya Missenyi.



3.2.1 Mifugo

Halmashauri imeendelea kuhakikisha kwamba, sekta ya Mifugo inaimarika na kuendelezwa kutokana na kuwa, maeneo makubwa yaliyotengwa rasmi kwa ajili ya Shughuli za ufugaji wa kisasa na fursa ya Sekta hii inayochangia shughuli za kiuchumi, pato la Wilaya na Ajira kwa Wananchi. Sekta ya Mifugo katika kipindi hicho imepata mafanikio yafuatayo:-

- i. Ruzuku ya dawa za kuogeshea mifugo imetolewa ambapo lita **123.5** za dawa zenyet thamani ya Tshs.**4,940,000.00** zimenunuliwa nakuwezesha wananchi kuchangia ghamama kidogo za uogeshaji ikiwa Ng'ombe **2,637**, Mbuzi **347**, Kondoo **123** wameogeshwa.
- ii. Dozi **37,000** za Chanjo ya Homa ya Mapafu ya Ng'ombe na dozi **5,600** za chanjo ya mbwa zimenunuliwa, kusambazwa na kutumika katika kata zote **20** za Wilaya kwa kipindi cha miaka mitano.
- iii. Ng'ombe **36,391** wamechanjwa dhidi ya Ugonjwa wa Homa ya Mapafu, na Mbwa **5,206** wamechanjwa dhidi ya Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa.
- iv. Ng'ombe **12,346** wamechanjwa dhidi ugonjwa wa homa ya Miguu na Midomo.
- v. Ujenzi na ukarabati wa josho moja la Kihororo umefanyika, ujenzi wa mnada wa mifugo wa Nkerenge na Bubale umefanyika pamoja na ukarabati wa machinjio ya Bunazi. Miundo mbinu mingine ni ukarabati wa Kituo cha Wakulima na Wafugaji Kayanga na uchimbaji wa malambo ya mifugo **17**.
- vi. Uzalishaji wa mazao ya mifugo umeongezeka kutoka Tani za nyama **474**, Mwaka 2015/2016 hadi Tani **517** mwaka 2019/2020 sawa na asilimia **9** ya malengo.
- vii. Uzalishaji wa maziwa ya Ng'ombe umeongezeka kutoka lita za maziwa **9,972,984** mwaka 2015/2016 hadi kufikia lita **12,252,626** Mwaka 2019/2020 sawa na wastani wa asilimia **27**.
- viii. Huduma ya mafunzo ya ufugaji bora na wenyetija yametolewa kwa Maafisa Mifugo **23** na wafugaji **449** kwa ajili ya kuboresha ufugaji.
- ix. Uhimilishaji umeongezeka kutoka Ng'ombe **231** mwaka 2015/2016 hadi Ng'ombe **694** mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia **200**.
- x. Ng'ombe **wapatao 55,479** kati ya **64,724** wamepigwa chapa mwaka 2017/2018 ikiwa ni hatua za utambuzi wa mifugo ili kuzuia mifugo haramu kutoka Nchi jirani.



Baadhi ya Ng'ombe aina ya Borani wakiingia kwenye josho la kisasa katika Shamba la Bubale

3.2.2 Uvuvi

Halmashuri ina maeneo yeye wingi wa rasilimali za uvuvi ambazo ni Sehemu ya Ziwa Victoria, Mto Kagera, Mto Ngoni, maeneo Oevu na Mabwawa ya ufugaji wa Samaki, Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita mafanikio yafuatayo yamepatikana katika sekta hii:-

- i. Vyombo vya uvuvi vilikuwa **36** mwaka 2015/2016 na hadi kufikia mwaka 2019/2020 vimekuwa **62** sawa na ongezeko la asilimia **72**. Aidha ongezeko hili limeongeza malipo ya fedha za Leseni,
- ii. Ajira za Uvuvi zimeongeka kutoka **217** mwaka 2015/2016 hadi kufikia ajira **274** mwaka 2019/2020,
- iii. Samaki tani **49** zenyet thamani ya Tsh. **245,000,000.00** walivuliwa kwa mwaka 2015/2016 na samaki Tani **120.2** zenyet thamani Tshs **721,452,000.00** walivuliwa kwa mwaka 2019/2020. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia **143**.
- iv. Sekta hii ya Uvuvi imechangia mapato ya Halmashauri kiasi cha Tshs **5,518,600.00** kwa mwaka 2015/2016 ukilinganisha na kiasi cha Tshs **19,533,400.00** kwa mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia **254**.
- v. Mabwawa ya ufugaji wa Samaki yameongezeka kutoka **25** mwaka 2015/2016 hadi **51** mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia **104**.



Baadhi ya Mabwawa ya kufugia Samaki katika shamba la Kashalu Kata Mutukula

- vi. Usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika ziwa victoria umeimarishwa ambapo, Kwa kipindi cha miaka 5, Doria za kawaida **22** zimefanyika kwa lengo la kudhibiti uvuvi haramu na kuthibiti upotevu wa maduhuli ya mapato ya Serikali katika maeneo mbalimbali ambapo zana haramu, nyavi **963** zenyet thamani ya Tshs. **95,616,000.00** zimeteketezwa.



3.3 Maliasili

Katika kipindi cha miaka mitano, pamoja na changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika Sekta ya Maliasili, Halmashauri imechukua hatua za kuhakikisha kuwa sekta hii inapewa msukumo wa kutosha ili kuhifadhi na iweze kuchangia kikamilifu katika kuboresha mapato ya Halmashauri. Hivyo katika kutimiza azma hiyo, Halmashauri imetekeliza yafuatayo:-

- i. Kwa kipindi cha miaka **mitano**, Mizinga ya nyuki **1,264** imetengenezwa na vikundi na watu binafsi na kufikisha jumla ya **1,673** ambapo **1,245** ni ya kisasa na **428** ni ya asili ikilinganishwa na mizinga **409** mwaka 2015,
- ii. Wanavijiji **472** wamepatiwa mafunzo ya mbinu za kisasa za ufugaji nyuki na kutafuta masoko ya asali ikiwa ni pamoja kuwawezesha kushiriki katika maonesho mbalimbali ndani na nje ya Wilaya.



Mizinga ya kisasa ya kufugia nyuki - Nsunga



Shamba darasa la ufugaji wa nyuki wa kisasa - Gera

- iii. Wastani wa upandaji miti kwa lengo la utunzaji wa mazingira umeongezeka kutoka miti **1,845,848** mwaka 2015/2016 hadi miti **2,320,116** mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia **26**. Aidha Jumla ya miti **11,084,302** imepandwa toka 2015/2016 hadi 2019/2020. Miti hii imepandwa na Taasisi, vikundi na watu binafsi.

Jedwali 3. Takwimu za Upandaji miti kuanzia 2015 - 2020

Na.	Mwaka	Watu Binafsi	Vikundi	Taasisi	Jumla
1.	2015/2016	1,312,952	212,002	320,894	1,845,848
2.	2016/2017	2,132,767	257,690	420,645	2,811,102
3.	2017/2018	1,432,539	285,850	280,158	1,998,547
4.	2018/2019	1,542,678	285,852	280,159	2,108,689
5.	2019/2020	1,826,219	301,006	192,891	2,320,116
6.	JUMLA	8,247,155	1,342,400	1,494,747	11,084,302

3.4. Usafi na Mazingira

Katika kipindi cha miaka mitano, Sekta ya Usafi na mazingira imeimarishwa ili kuongeza usimamizi, kiwango cha usafi, utunzaji na uhifadhi wa mazingira kwa Wananchi katika Wilaya yetu. Katika kutimiza azma hiyo, Halmashauri imefanikiwa kutekeleza mambo yafuatayo;

- Vizimba vyta kuhifadhi taka vimeongezeka kutoa **sifuri** mwaka 2015 hadi kufikia **tatu** mwaka 2020 na kujengwa katika mji wa Kyaka na Bunazi.



Mikokoteni ya kuzolea takataka - Bunazi



Kizimba cha kukusanya taka - Soko la Bunazi

- Sheria ndogo ya mwaka 2018 ya usimamizi wa takataka katika Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi imetungwa.
- Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi kuwa **mshindi wa tatu Kitaifa** katika mashindano ya Kampeini ya kitaifa ya usafi wa Mazingira ya mwaka 2019. Pamoja na **Kijiji kitobo kuwa mshindi wa tatu katika Mashindano ya Kitaifa** kwa uhamasishaji wananchi juu ya ujenzi wa vyoo bora.



Mhe. William Mtayoba, Diwani wa Kata ya Kitobo - Akipokea Cheti cha Ushindi wa Tatu wa Usafi wa Mazingira Kitaifa - Dodoma



- iv. Halmashauri imanzisha mfumo ada ya Taka katika miji ya Kyaka, Bunazi na Mutukula ambapo mapato yatokanayo na chanzo hiki ni kiasi cha Tshs **1,500,000** kwa mwezi. Aidha fedha hii imekuwa msaada mkubwa kwa kuwezesha shughuli za usafi.
- v. Idadi ya kaya zenyet vyoo bora zimeongezeka kutoka kaya **18,109** sawa na asilimia **37** kwa mwaka 2015 hadi Kaya **40,132** sawa na asilimia **82** mwaka 2020.
- vi. Idadi ya Vijiji vilivyo na kamati ya utunzaji na uhifadhi wa Mazingira imeongezeka kutoka Vijiji **41** sawa na asilimia **54** mwaka 2015/2016 hadi kufikia Vijiji **65** sawa na asilimia **85** Mwaka 2019/2020, Ongezeko hili ni sawa na asilimia **59** ya lengo.

3.4 Viwanda na Biashara

Utekelezaji wa sera ya uchumi wa Viwanda kuelekea uchumi wa kipato cha kati nchini umezingatiwa ambapo katika kipindi cha miaka mitano, Halmashauri ya Wilaya iliweka msukumo mkubwa zaidi kwa kuhamasisha na kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji wa Viwanda vipyta ili kuwezesha uwezo wa uzalishaji wa bidhaa za ndani kwa kuchukua hatua ya kutenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji Viwanda, Biashara na Kilimo yenye ukubwa wa zaidi ya hekta zaidi **5,250.5**, Kuandaa wasifu wa kiuchumi wa Wilaya, kutangaza fursa hizo za kiuchumi kwenye maonyesho ya kibiashara na kwenye Tovuti ya Halmsahauri.

Maeneon mbalimbali yametengwa kwa ajili ya shughuli za uwekezaji kamayanavyosomeka kwenye jedwali Na. 4.

Jedwali 4. Maeneo yaliyotengwa kwa uwekezaji.

Na	MAHALI ILIPO	ENEO Ha.	KATA
A Uwekezaji wa Kilimo			
1	Skimu ya Umwagiliaji Kyakakera	163	Kyaka
2	Byeju	500	Nsunga
3	Kajunguti	1000	Mushasha
4	Buchurago	2000	Bugorora
5	Skimu ya Umwagiliaji ya Nkenge	1054	Kitobo
6	Kabingo	500	Bugorora
B Uwekezaji kwenye biashara			
7	Kabakesa (Mpaka wa Tanzania na Uganda	8	Mutukula
8	Mutukula mjini (Mpaka wa Tanzania na Uganda (12972.45 M ²)	1.2	Mutukula
9	Eneo la Gulio(32948 M ²)	3.2	Bunazi
10	Stendi ya Magari (12800.28 M ²)	1.2	Kyaka
11	Eneo la Soko la kawaida(ekari 20)	8	Bugango
12	Mwalo wa Kabindi	1	Kashenye
13	Mnada wa Nkerenge (Ekari 10)	4	Mutukula
C Uwekezaji kwenye Viwanda			
14	Bwengabo – Kyaka Ekari 17.24 (Viwanja 4)	6.9	Kyaka
	JUMLA	5,250.5	

Idadi ya viwanda imeongezeka kutoka viwanda **61** (Kikubwa 1, vya kati 2 na vidogo 58) mwaka 2015/2016 hadi kufikia viwanda **98** (Vikubwa 2, Vya kati 5 na Vidogo 91) mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia **62**. Vile vile, idadi ya ajira katika viwanda hivyo imeongezeka kutoka ajira **1,620** mwaka 2015/2016 hadi kufikia ajira **2,040** mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia **79** Katika kipindi hiki cha miaka mitano.

Kiwanda kikubwa **kimoja** cha kukoboa kahawa cha Olam kimejengwa na kukamilika. Ongezeko hili limechangia kukua kwa sekta ya biashara kutoka asilimia **40** Mwaka 2015/2016 hadi asilimia **65** Mwaka 2019/2020.



Kiwanda cha uzalishaji wa Gypsum Board - Gera



4.0 HUDUMA ZA KIUCHUMI

4.1 Ardhi

Katika kipindi cha miaka mitano Halmashauri iliendelea na utoaji wa huduma za Sekta ya Ardhi ambapo mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

4.1.1 Utawala wa Ardhi:

- i. Jumla ya Vijiji **46** vimepatiwa vyeti vya Ardhi.
- ii. Jumla Vijiji **12** vimeandaliwa mipango ya matumizi bora ya Ardhikatika Halmashauri
- iii. Hatua za kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa lengo la kuondoa migogoro zimeendelea kuchukuliwa kwa kupima na kutoa hati miliki kwa wakulima na wawekezaji. Jitihada hizo zimewezesha upimaji wa jumla ya ekari **14,300** za mashamba.
- iv. Idadi ya viwanja vilivyopimwa imeongezeka kutoka **1,498** mwaka 2015/2016 hadi **2,552** mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia **70**.
- v. Jumla ya Hatimiliki za Kimila **715** zimetolewa kwa wanavijiji.
- vi. Upimaji wa mipaka baina ya vijiji na ranchi ya Missenyi umefanyika ili kutatua migogoro ya ardhi ya muda mrefu.

4.2 Barabara

Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya usafiri na Usafirishaji umeendelea kufanyika kwa lengo la kuchochea kukua kwa shughuli za kiuchumi, mawasiliano na kuongeza ajira katika Wilaya. Wilaya ina mtando wa barabara zenye urefu wa Km **921.16** kati ya hizo barabara za kiwango cha lami ni Km. **1.5**, Changarawe ni Km **260** na Udongo ni Km **659.66**. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Serikali imefanikiwa kutekeleza mambo yafuatayo katika sekta ya Barabara:-

- i. Barabara zenye urefu wa kilometa **656.93** zimekuwa katika hatua mbalimbali za ujenzi ambapo barabara zenye urefu wa kilometa **621.93** zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha udongo na changarawe.
- ii. Wilaya imepokea kiasi cha **Tsh.2,962,020,812.00** kwa ajili ya matengenezo ya barabara na madaraja madogo kwa kipindi cha miaka mitano.
- iii. Kwa mwaka 2019/2020 barabara zenye urefu wa kilometa **77.98 km** zimeendelea kujengwa kati ya hizo **1.6 km** ni kiwango cha lami kwa gharama ya Tshs. **741,972,480** ikiwa ni ahadi ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Jimbo la Nkenge na **76.36 km** ni kiwango cha changarawe na udongo kwa gharama ya Tsh. **407,521,200**. Barabara ambazo zinaendelea na matengenezo kwa kiwango cha lami ni **1.6 Km** katika mji wa Bunazi na barabara zilizopo katika hatua mbalimbali katika kiwango cha Changarawe na udongo ni katika kata **12** za Kanyigo, Kashenye, Kassambya, Kyaka, Kilimile, Buyago, Ruzinga, Kitobo, Ishozi, Ishunju, Mabale na Gera.



Ujenzi wa barabara ya Wanja wa Mashujaa - NMB kijiji cha Bunazi kwa kiwango cha lami km1.6

- i. Jumla ya makalvati (Madaraja madogo) **21** yamejengwa katika mtandao wa barabara mbalimbali za Wilaya,
- ii. Jumla ya barabara zenye urefu wa kilometra **60 km** zimefanyiwa upembuzi na usanifu kwa ajili ya ujenzi ikiwa **4 km** ni za lami ya Kyabaile na **56 km** ni barabara za udongo na changarawe. Barabara zilizokamilishwa ni kama zilivyoanishwa awali.
- iii. Matengenezo ya barabara hizi yametoa ajira kwa Wananchi **127** katika maeneo mbalimbali ya Wilaya.

4.3 Nishati ya Umeme

Kwa kutambua umuhimu wa nishati ya umeme kwa maendeleo ya Wananchi, katika kipindi cha miaka mitano, Serikali imechukua hatua za kuhakikisha kuwa nishati ya umeme inapatikana kwa wananchi kwa lengo la kukidhi mahitaji ya jamii, Aidha, kiwango cha uunganishwaji wa umeme vijiji kiwilaya umeongezeka kutoka Vijiji **26** sawa na asilimia **33.7** mwaka 2015/2016 hadi Vijiji **72** sawa na asilimia **93.5** mwaka 2019/2020. Jumla ya nyumba za makazi **3,326** nyumba za ibada **26** shule **43** na Zahanati **11** zimepatiwa umeme kupitia Mradi wa REA.



5.0 HUDUMA ZA JAMII

Huduma bora za jamii za Afya, Elimu, Maji na nyinginezo ni nyenzo muhimu katika kuondoa umasikini na kuharakisha maendeleo ya Wananchi. Katika kipindi cha miaka mitano zimefanyika, jitihada za kuhakikisha kwamba wananchi wanaendelea kunufaika na huduma hizo. Hivyo, Halmashauri imeendelea kupata mafanikio ya kutoa huduma za jamii ambazo ni za msingi katika kuboresha maisha ya Wananchi.

5.1 Afya

Ili kujenga Taifa lenye watu wenye Afya bora na wanaoweza kuzalisha mali na kutoa huduma mbalimbali, katika kipindi cha mwaka 2015-2020, Halmashauri imeendelea kutoa kipaumbele kwa kuzingatia maeneo yaliyoainishwa katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015-2020, ambapo mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

- i. Vituo vya kutolea huduma ya Afya vimeongezeka kutoka **36** mwaka 2015 hadi vituo **38** mwaka 2020.
- ii. Kliniki zinazohamishika (huduma za mkoba) za mfumo wa utoaji wa huduma kwa wazazi zimeongezeka kutoka **35** hadi kufikia kliniki **95**.
- iii. Vituo vya afya vimeongezeka kutoka **moja** kwa mwaka 2015/2016 hadi vituo **vitatu**, Mwaka 2019/2020.



Kituo cha Afya - Kabyaile kata ya Ishozi ni kituo kipyaa kilicho jengwa

- iv. Zahanati zimeongezeka kutoka **32** mwaka 2015/2016 hadi **33** mwaka 2019/2020.
- v. Watumishi wa kada ya afya wameongezeka kutoka **271** mwaka 2015/2016 hadi **382** mwaka 2019/2020.
- vi. Zahanati **22** zimekarabatiwa kuititia fedha za RBF ambapo jumla Tshs. **220,000,000.00** zimetumika, ambapo miundombinu iliyojengwa ni pamoja na upakaji rangi, ujenzi wa vichomea taka (incenirator) na ujenzi wa shimo la kutupia taka (Placenta pit).
- vii. Ujenzi/ukarabati wa kituo cha Afya Bunazi umefanyika ikiwa ni ujenzi wa wodi ya wazazi, Nyumba ya mtumishi, jengo la kuhifadhia maiti, ujenzi wa njia ya kuunganisha majengo, pia ukarabati wa jengo la wangojwa wa nje, chumba cha upasuaji na wodi moja ambapo jumla ya Tshs. **437,950,350.00** zimetumika. Aidha huduma ya upasuaji wa kinamama wajawazito imeanza kutolewa baada ya ujenzi na ukarabati huu kukamilika.



Ukarabati na Ujenzi wa Miundombinu ya Kituo cha Afya Bunazi.

- viii. Bajeti ya dawa na vifaa tiba imeongeze kakutoka Tshs.**281,763,765.00** mwaka 2015/2016 hadi kufikia Tshs.**593,837,525.6** mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilima **111**. Hii imeongeza upatikanaji wa dawa muhimu na vifaa tiba kutoka asilimia **73** mwaka 2015 hadi asilimia **97** mwaka 2019, dawa za VVU, kifua kikuu na malaria kwa asilimia **100** na hutolewa bure.
- ix. Jumla ya Wataalamu **15** wa Sekta ya Afya katika ngazi ya Halmashauri wamepata mafunzo ya uingizaji na utumiaji wa taarifa kupitia mfumo wa elektroniki ili kufanikisha upatikanaji wa takwimu za Afya ambapo jumla ya kompyuta **sita** kwa ajili ya Halmashauri na kompyuta **tatu** kwa ajili ya matumizi ya mfumo wa vituo zimetolewa;
- x. Kupitia mpango wa hati punguzo, vyandarua **4,309** vyenye viuutilifu kwa ajili ya kaya zenyet watoto chini ya miaka mitano, vyandarua **23,299** kwa ajili ya wajawazito na vyandarua **19,796** kwa ajili ya watoto chini ya umri wa mwaka mmoja vimesambazwa bure kwa lengo la kuboresha tiba ya malaria, kudhibiti mbu na kutoa kinga. Aidha, vyandarua **117,199** viligawiwa kwa wananchi bila malipo kupitia kampeni zilizolenga watoto chini ya miaka mitano na ngazi ya Kaya. Matokeo yake ni:-
- xi. Vifo vitokanavyo na malaria vimepungua kutoka **39** mwaka 2015 hadi kufikia **tisa** kwa kila watu **100,000** mwaka 2019 sawa na asilimia **333.3**.
- xii. Idadi ya watu waliopatikana na malaria imepungua kutoka watu **306** mwaka 2015 hadi **96** kwa kila watu **1,000** mwaka 2019 sawa na asilimia **69**.
- xiii. Mpango wa Upuliziaji wa viuutilifu ukoko katika kuta ndani ya nyumba ili kuua mbu wanaoeneza malaria umetekelzeza kwa vijiji **77** ambapo zaidi ya kaya **49,202** zenyet watu **222,714** zilinufaika;
- xiv. Vifo vyta watoto chini ya miaka **mitano** vimepungua kutoka **104** mwaka 2015 hadi **84** mwaka 2019 sawa na punguzo la asilimia **19**.



- xv. Vifo nya akina mama wajawazito vimepungua kutoka **10** mwaka 2015 hadi kufikia **nane** mwaka 2019 sawa na punguzo la asilimia **20**.
- xvi. Kiwango cha udumavu kwa watoto chini ya miaka **mitano** kimepungua kutoka asilimia **41.7** mwaka 2015 hadi kufikia asilimia **39.8** mwaka 2019.
- xvii. Jumla ya wazee **8,538** wamepatiwa huduma katika makazi kutoka wazee **1,120** mwaka 2015 hadi kufikia **8,538** mwaka 2019.
- xviii. Wananchi **1,611** sawa na asilimia **mbili** ya kaya **48,642** wamejiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) kufikia mwaka 2019.
- xix. Mpango wa kutokomeza maambukizi mapya ya Virusi nya UKIMWI (VVU) kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto umeanzishwa. Hadi sasa akina Mama walioanzishiwa tiba ni **144** kati ya mama wajawazito wa VVU watarajiwa **146**. Mpango huu umewezesha kiwango cha maambukizi kupungua kutoka asilimia **nne** mwaka 2015 hadi asilimia **1.6** mwaka 2020.

5.2 Elimu

5.2.1 Elimu Msingi

Katika kipindi cha miaka mitano, Halmashauri imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuboresha, kuimarisha na kupanua Elimu ya Awali kwa lengo la kuhakikisha kwamba elimu katika ngazi zote inakuwa na ubora unaostahili ili kuwawezesha vijana na makundi mengine kumudu ushindani wa soko la ajira na kuweza kujajiri wenywewe. Katika kipindi hicho, yamepatikana mafanikio yafuatayo:-

5.2.1.1 Elimu ya Awali

- i. Idadi ya shule za Msingi za Serikali zenyе madarasa ya Elimu ya Awali imeongezeka kutoka shule **95** mwaka 2015/2016 hadi shule **96** mwaka 2019/2020, sawa na ongezeko la asilimia **1.04**.
- ii. Idadi ya matundu ya vyoo imeongezeka kutoka **915** mwaka 2015/2016 hadi **1,001** mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia **8.6**.

5.2.1.2 Elimu ya Msingi

- i. Kupitia mpango wa kuwajengea uwezo walimu, jumla ya walimu **190** katika shule **95** walihusika. Walimu hao ni wa masomo ya Hisabati na Lugha na wamejengewa uwezo kuhusu mtaala ulioboreshwa.
- ii. Ruzuku ya Wanafunzi (Capitation Grants) imeendelea kutolewa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa nya kufundishia na kujifunzia katika shule zote. Ruzuku (Elimu bila malipo) tangu kuanzishwa Desemba, 2015 hadi April, 2020 zimetolewa jumla ya Tshs. **1,922,702,700.72**.

- iii. Uandikishaji wa wanafunzi wenyewe ulemavu imeongezeka kutoka wanafunzi **24** mwaka 2015 hadi wanafunzi **31** mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia **23**.
- iv. Uandikishaji wa wanafunzi umeongezeka: - Awali kutoka **6,116** Mwaka 2015 hadi **7,686** Mwaka 2020 sawa ongezeko la asilimia **20.4**, Darasa la kwanza kutoka **6107** Mwaka 2015 hadi **6,993** (2020) sawa na ongezeko la asilimia **13**.
- v. Uwiano wa kitabu kwa wanafunzi umeboreshwa kutoka kitabu kimoja wanafunzi **sita** mwaka 2015 kufikia wastani wa kitabu kimoja kwa wanafunzi **4** mwaka 2020.
- vi. Idadi ya nyumba za walimu imeongezeka kutoka **205** mwaka 2015 hadi **217** mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia **5.5**.
- vii. Idadi ya matundu ya vyoo imeongezeka kutoka **1,026** mwaka 2015 hadi **1,087** mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilima **sita**.
- viii. Madawati yameongezeka kutoka **14,022** mwaka 2015 hadi **19,987** mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia **30**.



Madawati katika shule ya Msingi Mutukula

- ix. Idadi ya vyumba vya madarasa imeongezeka kutoka **652** mwaka 2015 hadi **687** mwaka 2020. Ongezeko hilo la vyumba **35** vya madarasa ni sawa na asilimia **sita**.



Vyumba vya Madarasa Shule ya Msingi Kimkunda



- x. Madai mbalimbali ya walimu yameendelea kulipwa baada ya kuhakikiwa, ambapo jumla ya madai ya walimu yenye Tshs. **219,391,388.46** yamelipwa kati ya hizo, Tshs. **37,082,588.46** ni mishahara na Tshs **182,308,800.00** ni madeni mengine.
- xi. Jumla ya shule za msingi **72** kati ya shule **108** sawa na asilimia **67** zilikaguliwa mwaka 2020 ukilinganisha na mwaka 2015 zilipokaguliwa shule **54** kati ya shule **102** sawa na asilimia 53 kwa lengo la kuboresha kiwango cha elimu.
- xii. Ufaulu katika Mitihani ya kumaliza Elimu ya Msingi umeongezeka kutoka asilimia **75.5** mwaka 2015 hadi kufikia asilimia **84.8** mwaka 2020. Hili ni Ongezeko la asilimia **9.3**.
- xi. Ujenzi wa ofisi ya Mdhibiti Ubora wa Shule katika Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi Tsh. **152,000,000.00**



5.2.1.3 Elimu ya Mafunzo ya Ufundi

Udahili wa wanachuo katika chuo cha ufundi Stadi Gera umeongezeka kutoka wanachuo **43** mwaka 2015 hadi kufikia wanachuo **173** mwaka 2020 ikiwa ni ongezeko la asilimia **302**.

Ongezeko hili limetokana na ukarabati wa miundombinu ya chuo ambayo ilikuwa katika hali ya uchakavu. Ukarabati huo umehusisha madarasa, mabweni na jengo la utawala kwa gharama ya **Tsh.514,000,000.00** kutoka Serikali Kuu. Vile vile Chuo kimeweka miundombinu ya ufügaji nyuki kwa gharama ya **Tsh. 130,210,000.00** kwa ajili ya mafunzo hayo kwa vijana.

5.2.2 Elimu ya Sekondari

- i. Idadi ya walimu wa sekondari imeongezeka kutoka **242** mwaka 2015 hadi walimu **379** mwaka 2020. Pia walimu wa ziada wapatao **96** wa masomo ya sanaa kuhamishiwa shule za msingi,
- ii. Walimu wa masomo ya Sayansi wameongezeka kutoka **54** mwaka 2015 hadi kufikia **90** mwaka 2020, ikilinganishwa na mahitaji ya walimu **162** wa masomo ya Sayansi.

